

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS-TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA TUNDURU**

**TANGAZO LA ZABUNI**



06 March, 2018.

**UFUNDI WA UJENZI WA KITUO CHA AFYA MATEMANGA**

Halmashauri ya wilaya ya Tunduru ilitangaza tangazo la kazi ya ufundi wa kituo cha afya Matemanga unaotarajia kuanza hivi karibuni. Tangazo hilo lilitangazwa mnamo tarehe 26/02/2018 hadi tarehe 07/03/2018 ambapo ilikua ni ukomo wa kuwasilisha maombi hayo.

Hata hivyo Halmashauri imeamua kuongeza muda wa ukomo wa kuwasilisha maombi ya ujenzi huo hadi tarehe 12/03/2018, Hii itasaidia kupata wigo mkubwa kwa mafundi wa maeneo mbalimbali (hasa vijijini) kuweza kuomba kazi hizo.

Aidha maelekezo ya awali ya tangazo hilo yatabaki vilevile isipokua kwa kipengele cha muda tu.

**MKURUGENZI MTENDAJI**  
**HALMASHAURI YA WILAYA**  
**TUNDURU**

**MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA**  
**TUNDURU**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS-TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA TUNDURU**



26 / 02 / 2018

**TANGAZO LA KAZI ZA UFUNDI WA UJENZI WA KITUO CHA AFYA MATEMANGA**

1. Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru imepokea fedha kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ajili ya ujenzi na ukamilishaji wa kituo cha Afya Matemanga.
2. Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru anawatangazia wananchi wote wenye uwezo, sifa na uzoefu wa kufanya kazi za ufundi wa kujenga majengo ya Serikali kuomba kazi ya ufundi wa ujenzi ambazo zitafanyika katika kituo cha Afya Matemanga.
3. Tangazo hili linapatikana kwenye mbao zote za matangazo kituo cha afya Matemanga na mbao zote za matangazo za Halmashauri ya Wilaya Tunduru.
4. Mafundi walio na sifa na uwezo wanaweza kupata taarifa kuhusu taarifa hizi kwenye ofisi ya Katibu wa Bodi ya Zabuni, Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru S.L.P 275, Tunduru. Ofisi Na. 35 au 36 kuanzia saa 2.30 asubuhi hadi saa 9.30 alasiri, Jumatatu hadi Ijumaa isipokuwa siku za sikukuu.
5. Nyaraka nyingine zinazohusiana na tangazo hili ( michoro na mchanganuo wa kazi zitakazofanyika) zinapatikana ofisi ya Katibu wa Bodi ya Zabuni .
6. Baada ya fundi kupata mchanganuo wa kazi za kufanya na michoro , anatakiwa kuwasilisha maombi yake kwa maandishi kwa Mkurugenzi Mtendaji, Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru S.L.P 275, Tunduru akionesha gharama halisi za ufundi kwa kazi ya jengo analoomba kazi ya kujenga kulinga na mchoro.
7. Halmashauri kwa kushirikiana na kamati ya ujenzi itanunua vifaa/bidhaa na fundi atakuwa na jukumu la kufanya ujenzi na kazi nyingine zitakazoainishwa na msimamizi wa ujenzi.

8. Majengo yanayotarajiwa kujengwa ni kama ifuatavyo:-
- Jengo la Upasuaji (Theatre)
  - Wodi ya kina mama (Female ward)
  - Wodi ya watoto (Children's ward)
  - Maabara (Laboratory)
  - Nyumba ya mtumishi inayojitegemea (Staff house)
  - Chumba cha kuhifadhia maiti (Mortuary)
  - Kichomea taka (Incinerator) na shimo la kutupia kondo la nyuma (Placenta pit)
9. Sifa za mwombaji ( Local Fundi's ) :-
- Mwombaji awasilishe vielelezo vya kuonyesha sifa , uwezo na uzoefu wa kujenga majengo ya Serikali. Awasilishe viambatanisho vyote muhimu vya sehemu zote alizofanya kazi.
  - Awe na uwezo wa kutafsiri michoro (drawings) pamoja na maelezo mengine ya kitaalam (specifications).
  - Awe na uwezo wa kufanya kazi kwa kuzingatia kanuni na taratibu za Serikali (Mzalendo na Mwaminifu)
  - Awe Mtanzania Mwenye umri usiopungua miaka 18
  - Ajue kujenga kwa mawe na tofali
  - Ajue luweka sakafu vizuri
  - Ajue kuseti jengo na kunyoosha kuta na nguzo vizuri
  - Ajue kumaliza lip (Skimming)
  - Ajue kuchanganya saruji na mchanga.
10. Maombi yote yawasilishwe kwenye nakala halisi moja na nakala mbili (2) kivuli (copy) yakiwa yamefungwa vizuri. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 7/3/2018 saa 8:00 mchana.
11. Maombi yatakayoletwa kwa kuchelewa au yakiwa hayajafungwa hayatapokelewa kwa ajili ya ufunguzi.

  
MKURUGENZI MTENDAJI (W)

TUNDURU

MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA  
TUNDURU